

[Inicio](#) > [Ukweli Wa Shia Ithna Ashariyyah](#) > Dibaji Ya Mtarjum

Dibaji Ya Mtarjum

Mtunzi wa kitabu hiki Haqiqat Shi'a Ithna-'Ashariyyah amejitahidi sana kutoa ushahidi wa hoja zake katika Kitabu cha Sahih Al-Bukhari na hiyo ni kutokana na uzito na umuhimu wa Kitabu hicho ambacho kinazingatiwa na ndugu zetu Ahl as-Sunnah wal Jama'a kuwa ni Kitabu Sahih zaidi baada ya Kitabu cha Allah (s.w.t.).

Na yaonyesha kuwa Mtunzi amenukuu ushahidi wake kutoka Sahih Al-Bukhari (Arabic-English) cha Dr. Muhammad Muhsin Khan-chapa ya Dar al-Arabia Beirut.

Ama kuhusu Sahih zingine kama vile Sahih Muslim na nyinginez, Mtunzi ametaja ni mlango na maudhui gani amenukuu ushahidi wake jambo ambalo halitamwia vigumu msomaji kufuatilia pindi atakapopenda kufanya hivyo.

Ni matumaini yetu kuwa - wasomaji wetu watavutiwa na mtiririko wa Kitabu hiki; pili, watakuwa ni wadadisi, waadilifu na wapambanua haki na batili. Hivyo hawatakanusha au kukubali jambo bila ya ushahidi wowote.

Tunamwomba Allah (s.w.t.) atuonyeshe njia ya haki na atujaalie kuifuata na atuonyeshe njia ya mfarakano na atujaalie kuiepuka.

Wabillaahi Taufiq.

Abdul Karim J. Nkusui

27/11/2001

URL del envío: <http://www.al-islam.org/es/node/25148>